BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

MEI, 2025

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS – SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninachukuwa fursa hii adhim kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwenye wingi wa Rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika mkutano huu wa Kumi na Tisa kwa ajili yakujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali yam waka wa fedha 2025/2026. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutekeleza jukumu hili kwa mafanikio makubwa. Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza vyema Baraza hili kwa hekma, busara na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nakuchukuwa fursa hii adhim kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu na mafanikio makubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema na uwezo ili aendelee kutumia hekma na busara zake katika kuisimamia Serikali na wananchi wake kwa kufuata misingi iliyowekwa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa manufaa ya nchi yetu. Aidha, kamati hii inampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuaminiwa na Chama Cha Mapinduzi kwa kuteuliwa tena kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar kwenye uchaguzi mkuu wa 2025 – 2030 kupitia Chama cha Mapinduzi, kamati yetu inamtakia ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati yetu inampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi zake na maarifa yake makubwa katika kushauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kutekeleza majukumu yake ya kila siku, tunamuomba Mwneyezi Mungu amzidishie hekma na busara katika kuyafikia makusudio yake, kwa hakika Mheshimiwa Makamo wa Pili ameitendea haki nafasi yake hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Islam Seif Salum bila ya kuwasahau watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii. Kamati inawashukuru na kuwapongeza kwa kuitayarisha bajeti hii kwa ufanisi mkubwa kwa kufuata na kuonesha vipaumbele vikuuvya nchi ambavyo ndio msingi wa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa heshima na taadhima, naomba kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu ambao wamejitoa kwa nguvu zote kupitia na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026,kwa muktadha huo naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Maryam Thani Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
4.	Mhe. Jamal Kassim Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Suleiman Haroub Suleiman	Mjumbe
6.	Mhe. Haji Shaaban Waziri	Mjumbe
7.	Mhe. Abdallah Abass Wadi	Mjumbe
8.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
9.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
10.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu
11.	Ndg. Shawana Mohammed Haji	Katibu
12.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo mfupi sasa naomba kutumia fursa hii kutekeleza jukumu langu la msingi lililonileta mbele ya kiti chako.

Mheshimiwa Spika,Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu wa Baraza la Wawakilishi inatekeleza kazi za kawaida na kazi za miradi ya maendeleo kupitia Mafungu matatu ya kibajeti ambayo ni Fungu C01 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, fungu C 02 Afisi ya Baraza la Wawakilishi na fungu C 03 Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Mafungu yote haya yanatekeleza kazi zake kupitia Programu kuu *Saba (7)* na programu ndogo *14* ambazo zinasimamiwa na Idara *saba (7)* na Taasisi *Tatu (3)*.

FUNGU C 01: AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mheshimiwa Spika, kupitia programu ndogo [SC010201] ya kukabiliana na maafa yenye jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa sera ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar ambayo inalenga kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa. Kamati inaipongeza Kamisheni ya Maafa kwa kutekeleza vyema malengo yake ya mwaka 2024/2025 kwa kujikita zaidi kwenye kutoa elimu na mafunzo ya kujikinga na maafa katika jamii. Kamati inaishauri Serikali kuipatia bajeti hii tunayoenda kuipitisha

kusaidia kutoa nyenzo za kutosha kwa Kamisheni ili kuwa na nguvu za kukabiliana na maafa pamoja na kuondosha viashiria vyote ambavyo vitapelekea kutokea kwa maafa katika jamii. Aidha, kamati kwa mara nyengine tena inaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa maafa ambao utasaidia kupatikana fedha za haraka wakati wa kutokea maafa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu ndogo [SC010202] – Sherehe za Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yenye jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi viongozi wa kitaifa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwapatia fedha zaidi ya malengo katika kutekeleza kazi zake ambapo kwa kipindi cha miezi tisa (julai – Machi 2024/2025) wamepatiwa fedha wastani wa aslimia 118 kati ya bajeti waliyotengewa. Hivyo, Idara hii imeweza kutekeleza vyema majukumu yake na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Idara hii katika wiki ya kuwaenzi viongozi ambayo hufanyika kila ifikapo mwezi wa Aprili ya kila mwaka kuboresha zaidi wiki hii kwa kutoa elimu na hamasa kwa umma ili iweze kufahamika na kila mmoja wetu mchango wa waasisi wa Mapinduzi na viongozi mashuhuri kutoka Zanzibar. Aidha, idara iandae makala maalumu ambayo itaelezea historia ya waasisi wa mapinduzi na watu mashuhuri wa nchi yetu ambao wamepitia vipindi tofauti katika historia za Visiwa hivi. Aidha, Makala hizi zitangazwe kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na wanafunzi wa skuli za misingi, sekondari na elimu ya juu kwa lengo la kufahamu mchango wao mkubwa walioutoa katika historia na maendeleo ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, kupitia programu hii inaishauri Serikali kuziboresha barabara za ndani ambazo zimeenda kwenye makaburi ya viongozi wetu mashuhuri na waasisi wa Mapinduzi ambao wameshatangulia mbele ya haki ili kuifanya wiki ya kuwaenzi viongozi kuwa rahisi kuyafikia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika programu ndogo [SC010203] Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za Serikali. Kamati inazitaka taasisi za umma kuhakikisha wametekeleza vyema wajibu wao na kuzingatia masuala ya utawala bora kwa wananchi. Aidha, kamati inaipongeza Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa ushiriki wao mkubwa katika kuchangia pato la taifa. Shukrani za pekee ziende kwa Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar kwa namna anavyosimamia miradi mbali mbali ya ujenzi wa ofisi za Mikoa na Wilaya. Hata hivyo, Kamati inaishauri idara kusimamia kikamilifu ujenzi wa mradi wa ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi iliyopo Mazizini kutokana na mkandarasi wake kufanya kazi kwa kusuasua na kupelekea ujenzi huo kutomalizika kwa takriban miezi kumi sasa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii kumeifanya Kamati kuridhia utendaji wa idara ya uratibu Dodoma na Dar es Salaam kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Kamati pia, inaipongeza Serikali kwa kuandaa mpango wa kuwapatia usafiri wa uhakika ambao utaenda kuwa mkombozi wa maendeleo yao. Aidha, kamati inatoa pongezi zake za dhati kabisa kwa mradi wa TASAF kupitia mpango wa Kunusuru Kaya Masikini nchini kwa lengo la kupunguza umasikini uliokithiri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya Kamati hii tumepata mashirikiano makubwa na viongozi wa mfuko wa TASAF chini ya Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Shadrack Mzirai na wasaidizi wake kutoka Makao Makuu Dodoma, Zanzibar na Pemba kwa hakika kazi zilizofanywa na TASAF kwa upande wa Zanzibar zimeleta faraja kwa wananchi wa Zanzibar ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, ujenzi wa skuli, ujenzi wa madaraja na kutekelezwa kwa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini nchini.

FUNGU C02: BARAZA LA WAWAKILISHI

Mheshimiwa Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni kati ya Mihimili mikuu mitatu ya nchi, ambapo muhimili huu una jukumu kubwa la kutunga Sheria, kufuatilia utendaji wa Serikali na kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali ili kuhakikisha

kuwa mahitaji na maendeleo ya wananchi yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu kuu [C0201] – kutunga sheria, kupitisha bajeti na kusimamia taasisi za Serikali inahusika na utekelezaji wa jukumu la msingi la Baraza la Wawakilishi ambalo ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria vinatekelezwa ili kukuza demokrasia na uwakilishi wa wananchi wa Zanzibar. Kamati kupitia programu hii inaipongeza Afisi ya Baraza kwa kutekeleza vyema jukumu lake la msingi na inaitaka afisi kuzidisha juhudi katika kuzisimamia taasisi za umma kutimiza wajibu wao. Ili kufikia malengo ya programu, kamati inaishauri Serikali kuendelea kuipatia afisi vyombo vya usafiri kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake ya kila siku.

FUNGU C03: TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Mheshimiwa Spika,Tume ya Uchaguzi Zanzibar ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za uchaguzi hapa Zanzibar kupitia programu kuu mbili ikiwemo programu ya usimamizi wa kazi za utawala za uendeshaji wa shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Kamati inaipongeza Afisi ya Tume kwa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa jengo la Tume ya Uchaguzi Maisara ambao umezingatia malengo ya Tume na kwenda sambamba na matarajio yake kwa mujibu wa uzoefu wao kupitia nchi za Jumuiya ya Madola. Aidha, kamati inaipongeza Serikali kuanzisha ujenzi wa Ofisi za Wilaya kwa upande wa Unguja na Pemba mpango ambao umeanza kutekelezwa kwa kutafuta viwanja na kuvipatia hati za umiliki. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kusimamia na kutekeleza kwa wakati shughuli za ujenzi kwa zile Wilaya ambazo zimeshapata viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wilaya.

HITIMISHO:

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka huu wa 2025 ni mwaka wa uchaguzi, Kamati yangu inatoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kufanya uchaguzi kwa amani na upendo bila ya kuingiza nchi katika migogoro ya kisiasa. Aidha, kwa niaba ya Kamati yangu nawaombea kila la heri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waweze kuchaguliwa tena warudi Barazani, kipekee tunamuombea Rais wetu kipenzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ashinde kwa kishindo kwenye uchaguzi huu.

Mheshimiwa Spika, Dua maalumu ni kwako wewe Mhe. Spika ili nawe uweze kushinda nafasi ya uspika kwa mara nyengine uendelee kulingoza Baraza hili tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri kwamba katika mwaka ujao wa bajeti Serikali kujitahidi kuzipatia taasisi husika fedha ambazo Baraza limeridhia na kuwapitishia ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie bajeti hii na hatimae waidhinishie Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha *2025/2026* kama ilivyokusudiwa.
Mheshimiwa Spika, *kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,



(Machano Othman Said)
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
BARAZA LA WAWAKILISHI,
ZANZIBAR